



MAELEZO SAHIHI

MUONGOZO WA REDIO

MUONGOZO WA SHUGHULI ZA  
KIJAMII

---

# TASNIA YA CHAKULA

TANZANIA

## UTANGULIZI

Jinsi ya kulisha idadi ya watu bilioni 7.7 ulimwenguni vizuri, katikati ya shida ya mabadiliko ya tabia nchi na kuzorota kwa haraka kwa mazingira, ni moja ya changamoto muhimu na ngumu inayotukabili. Kwa njia nyingi, tasnia ya chakula inachangia kuzorota kwa mazingira, ukosefu wa usawa kwenye jamii na magonjwa ya binadamu: Ulimaji huharibu misitu ya asili na mbuga zenye utajiri wa viumbe-hai. Mbolea za kikemikali na dawa za wadudu hutumia nishati nyingi kuzitengeneza na huacha sumu kwenye udongo. Uvuvi wa viwandani unamaliza bahari, na kusababisha kupungua kwa idadi ya samaki wa mwituni ambao hutoa protini kwa mamilioni ya watu wanaoishi katika maeneo ya pwani ([Guardian](#)). Kwenye ardhi, ufugaji wa wanyama viwandani hutumia rasilimali nyingi za asili na hutoa uchafuzi unaodhuru maziwa, mito na bahari. Chakula husafirishwa mbali kupitia barabara, kutoka shambani hadi kufikia kwenye meza zetu, na huzalisha uchafu mwingi. Vyakula pia husindikwa viwandani kwa kutumia nishati na maji mengi, na kisha kupakiwa kwa kutumia plastiki, styrofoamu na vifaa vingine vinavyoathiri sayari. Chakula pia kinachezewa na kutupwatupwa (wasted) wakati wote katika mnyororo wa thamani: kuanzia wakati kinakua, kuvunwa, kusindikwa, kwenye jokofu, usafirishaji, upakiaji, katika maduka na tunapotupa kilicho kwenye sahani zetu.

Kwa miaka 50 iliyopita, chakula kimeendelea kuwa bidhaa ya kidunia, na hapo ndipo shida kubwa ilipo. Sawa na yale tuliona katika mtaala wa **Mavazi, Mitindo na Uuzaji**, utandawazi wa chakula unamaanisha kwamba watu wengi

hawazalishi chakula chao wenyewe au kula chakula kilichozalishwa ndani, ilhali wanategemea minyororo ya thamani ya chakula ambayo hathari zake hawazioni. Wakati zaidi ya nusu ya chakula duniani bado kinazalishwa na wakulima wadogo wadogo, wengi ambao wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa usalama wa chakula, kampuni kubwa za kimataifa zimeibuka na kuendelea kupata nguvu kwa kasi, kwa kutumia ukubwa, utajiri na nguvu yao ya kuunda mfumo wa chakula kwa njia ambazo zinawanufaisha, lakini zinaweza kuwa na madhara kwa watu na sayari. Hali hii inaongezeka kwa kasi kwasababu umiliki wa usambazaji wa chakula ulimwenguni upo mikononi mwa mashirika machache makubwa ya kimataifa. Uchafuzi wote, uzalishaji wa gesi chafu na taka zinazozalishwa na viwanda vya chakula unahatarisha afya ya binadamu pia. Lakini pia kuna taarifa nyingine mbaya: “chakula cha viwandani” kilichosindikwa zaidi hakina manufaa mengi kiafya - ukilinganisha na chakula kisafi, kilichozalishwa ndani/mtaani/nchini. Kimepakiwa na mafuta na kalori nyingi bila ya kuwa na virutubisho vingi-- na hii inachangia pakubwa kwa janga kubwa ulimwenguni la vitambi (obesity), ugonjwa wa kisukari na magonjwa ya moyo. Kwa kiasi kikubwa, tasnia ya chakula inazidi kutufanya kuwa wagonjwa na kuangamiza sayari. Kila nchi ya Kiafrika sasa inakabiliwa na mzigo wa mara tatu zaidi wa njaa, magonjwa ya utapiamlo (micronutrients deficiencies) (WWF-SA), wakati kimataifa, mtu mmoja kati ya watu watatu ana njaa au kitambi/mafuta mengi mwilini ([IPES-Food, Gordon 2017](#)).

## TAFSIRI YA MISAMIATI

- **Usalama wa chakula** unamaanisha kuwa na hela na rasilimali nyingine unazohitaji kupata chakula cha kutosha ili kudumisha hali hai na yenye afya ya maisha, ambayo pia inaendana na matakwa yako ya kitamaduni ([Food and Agriculture Organisation of the United Nations](#)). Usalama wa chakula hautegemei uzalishaji wa chakula tu, bali pia unategemea mwendelezo wa uwepo na

upatikanaji wa chakula kwa watu. Kilimo hutoa mchango muhimu sana kwa usalama wa chakula, ambao ni muhimu kwa afya na ustawi wa watu, uchumi na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, watu wengi wanaokumbwa na hali ya ukosefu wa chakula wana njaa sio kwa sababu chakula hakipatikani wanakoishi, lakini kwa sababu hawana uwezo wa kumudu gharama za chakula. FAO inaripoti kwamba

ukosefu wa chakula sasa unaongezeka barani Afrika kwa mara ya kwanza katika muongo mmoja, kwa sababu zinazojumuisha upoteaji wa mazao unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na kupanda kwa bei ya chakula (FAO).

- **Chakula cha viwandani** ni chakula kinachozalishwa na makampuni - mara nyingi makampuni makubwa ya kimataifa, wala sio kinachotokana na shughuli ndogo-ndogo au za ndani za kuzalisha chakula. Mfumo wa uzalishaji wa chakula cha viwandani unasisitiza usawa, viwango na wingi: aina moja ya chakula hupandwa kwa wingi kutumia pembejeo nyingi kwenye shamba kubwa, halafu husafirishwa ng'ambo, kusindikwa, kufungwa na kusambazwa kote, mara nyingi kimataifa, kwa maduka makubwa, minyororo ya chakula cha haraka na maduka mengine. Mtindo wa chakula cha viwandani umeleta kiasi kikubwa cha chakula kwa watu ulimwenguni kote, na kuwezesha upatikanaji wa kalori/nishati nyingi za chakula kwa watu wengi zaidi kuliko vile ilishawahi kutokea. Lakini ufanisi huu mkubwa umekuja kwa gharama kubwa kwa mazingira, afya ya binadamu na ustawi (IPES-Food).
- **Chakula kikubwa (Big food), au mashirika makubwa ya chakula**, ni biashara za kimataifa ambazo zinazidi kudhibiti mlolongo wa usambazaji wa chakula, kutoka mbegu na pembejeo zingine zinazotumiwa kwa ukulima hadi bidhaa za mwisho kwenye maduka makubwa (supermarket). Minyororo ya kimataifa ya usambazaji sasa imedhibitiwa na kampuni chache tu, na inawapa uwezo mkubwa wa kuamua jinsi chakula kinazalishwa, jinsi rasilimali zinavyotumiwa, jinsi wafanyakazi wa mashamba na viwanda hutendewa, na aina ya chakula ambacho watumiaji wanapata. Kwa mfano, miaka ishirini iliyopita kulikuwa na kampuni karibu 600 kubwa ulimwenguni kote zinazosambaza mbegu, dawa za viuadudu na mbolea. Sasa ni kampuni tatu tu ambazo zinadhhibiti nusu ya soko la mbegu duniani kote. Wakati

huo-huo, ni mashirika manne tu yanadhhibiti 70% ya biashara za kimataifa na bidhaa za kilimo (**Development + Cooperation**), na wanasambazia makampuni makubwa ya chakula ulimwenguni bidhaa kwa bei rahisi. Hayo maduka makubwa yananufaika kwa upendeleo huo ambao unazidi kuwapa utawala kwenye nafasi ya mauzo ya rejareja katika miji mikubwa zaidi barani Afrika.

- **Chakula cha afya** ni chakula ambacho hupandwa katika udongo msafi, wenye rutuba na ulioandaliwa na usindikaji mwepesi au mdogo tu, ili kutunza virutubisho vyake. Lishe yenye afya, kwa watu na sayari, ni **vyakula tofauti**, vyenye nafaka nzima, kunde, karanga, mbegu, matunda na mboga; na kiasi wastani cha nyama, samaki na maziwa (Eat-Lancet). Kwa bahati mbaya, mfumo wa chakula cha viwandani unasisitiza wingi badala ya ubora na utofautii: inakusudia kutoa kiwango kikubwa cha chakula cha bei rahisi, kisicho na afya. Kwa hivyo kwa wengi wetu, vyakula vya lishe bora vyenye afya mara nyingi huwa ghali na ni vigumu kuvipata kuliko vile vyakula vya bei rahisi vilivyosindikwa, haswa katika miji inayopanuka kwa kasi barani Afrika.
- **Chakula cha haraka (Fast food)** ni tasnia ya dola bilioni nyingi, inayotoa chakula kilichopikwa tayari, kilichozalishwa kwa wingi (kama vile 'hamburger' au kuku) kwa watumiaji. KFC, Burger King na biashara nyingine maarufu zinasambaa na kupanuka haraka katika miji ya Kiafrika, ikiwapa watu ufahari na urahisi. Kampuni hizi hutumia mamilioni ya dola kufanya matangazo na kutoa picha kwamba chakula cha haraka ni kizuri na watu wanapaswa kutamani kukila. Lakini chakula cha haraka kina athari nyingi kwa mazingira, kijamii na kiafya: ni sehemu ya mfumo wa chakula cha viwandani inayochangia uzalishaji wa gesi chafu na uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa ardhi kutoka kwa kilimo cha viwandani na viwanda, na kazi zinazolipa mishahara ya chini. Chakula cha haraka kwa ujumla pia kina mafuta zaidi, chumvi, cholesterol na sukari kuliko chakula kilichopikwa

nyumbani, kwa hivyo kinachangia magonjwa duniani, kama vile ugonjwa wa fetma (obesity), ugonjwa wa kisukari na magonjwa ya moyo.

- **Sera, kanuni na makubaliano ya biashara** ni nguvu zinazoelekeza jinsi watu wanavyopata chakula, na aina ya vyakula wanavyopata. Kwa mfano, makampuni makubwa ya chakula kama Nestle na Unilever hutolewa ruzuku kwa njia nyingi zinazowawezesha kuuza vyakula vyao kwa bei rahisi kwa watumiaji: wanapata mikopo ya riba ndogo na bidhaa za bei rahisi, kama vile mahindi; na wanaruhusiwa kulipa wafanyakazi mishahara midogo sana. Mara nyingi huwa hawawajibiki kwa kuchafua mazingira (Raj Patel). Wakati nchi za Kiafrika zinajadili makubaliano ya biashara na China,

nchi za Ulaya na Amerika ya Kaskazini, mara nyingi wanashinikizwa kukubali kupata ruzuku ya chakula, pembejeo na teknolojia kama vile GMO ambazo ni za bei rahisi sana, na ambazo wakulima na viwanda vya ndani hawawezi kushindana nazo.

Kwa sababu chakula kimekuwa bidhaa ya ulimwengu, bei ya chakula inaweza kuathiriwa na masoko ya kimataifa. Kuharibika kwa mazao, kuongezeka kwa bei ya mafuta, machafuko ya kisiasa na migogoro ya kibiashara katika sehemu zingine za ulimwengu inaweza kuathiri bei ya chakula katika maduka makubwa ya ndani. Kaya masikini haswa zinaweza kuathiriwa na mshtuko wa bei ya chakula, kwa sababu hawawezi kutumia pesa zaidi kwenye chakula wakati bei zinapongezeka. Basi, wataamua tu kukinunua kile chakula cha bei rahisi angalau 'wajaze tumbo', badala ya chakula bora chenye afya na usafi wa vyakula kamili, bila kujali athara kwa Dunia ([Joubert](#)).

**ONDOA HADITHI POTOFU (UZUSHI)****HADITHI (UZUSHI)**

Upatikanaji wa maduka ya chakula cha haraka kama McDonald's na KFC katika maduka mapya makubwa unapaswa kusherehekewa/ kupongezwa kama ishara ya maendeleo.

Njia bora ya kuiokoa sayari ni kila mtu awe mla mboga za majani tu (vegan).

Kaya ambazo zinakabiliwa na ukosefu wa usalama wa chakula zinatakiwa kuwajibika kwa maisha yao na kushughulikia kuboresha mapato ya familia zao ili waweze kukidhi mahitaji yao.

**UKWELI**


Viwanda vya chakula cha haraka hutumia mamilioni ya dola kuonyesha bidhaa zao kuwa za kuvutia na kupendeza. Lakini kwa kweli, chakula cha haraka ni kibaya kwa sayari kama tu kilivyo kwa afya yako. Sekta ya chakula cha haraka hutegemea sana nyama ya viwandani, ambayo hutumia karibu theluthi ya nafaka zote zinazozalishwa ulimwenguni kote, na ina alama kubwa ya matumizi ya maji (kwa mfano, inachukua lita 15,000 za maji ili kutoa kilo moja ya nyama, ikilinganishwa na lita 322 kutoa kilo ya mboga za majani, Guardian). Dawa za viwadudu pia hutumiwa mara kwa mara katika kilimo cha kibiashara cha mifugo, na kusababisha kuenea kwa upinzani mkubwa wa vijidudu (antimicrobial resistance). Uuzaji wa vyakula vya haraka mara nyingi pia hutumia wauzaji wa kimataifa badala ya wazalishaji wa ndani - kwa hivyo ikiwa utatumia pesa zako kwenye chakula cha haraka, unaondoa rasilimali mbali na uchumi wa ndani na njia za kuishi za wakulima wa hapa (Guardian).

Kulingana na ripoti ya tume ya Eat-Lancet, 'lishe ya afya ya sayari' kusaidia idadi ya watu bilioni 10 inaweza tu kupatikana kwa kupunguzwa kwa 90% ya nyama nyekundu na utumiaji wa maziwa. Lakini nyama na maziwa hazipaswi zipuuzwe kabisa. Kwa kweli, kilimo cha mifugo ni muhimu kwa mamilioni ya wakulima wadogo barani Afrika, na huwapatia faida nyingi, ikiwemo mbolea hai na pia vyanzo vinavyohitajika vya protini. Shida kuu na uzalishaji wa nyama na maziwa iko katika mfumo wa viwanda unaotumiwa kwa kilimo na uzalishaji wa chakula, ambao unasababisha uharibifu mkubwa wa ardhi, maji na mabadiliko ya tabia nchi.

Kuna ugumu katika sababu za ukosefu wa usalama wa chakula, lakini mara nyingi zina uhusiano mkubwa na mabadiliko ya tabia nchi, ukosefu wa kazi, kufanya chakula kuwa bidhaa ya kibiashara na shida nyingine za kijamii kuliko jukumu la kibinafsi. Kwa mfano, ukosefu wa masoko, upanuzi na msaada wa sera, pamoja na upotezaji unaotokana na mabadiliko ya tabia nchi na bei ya chini inayotolewa na wanunuzi, inawasukuma mamilioni ya wakulima wadogo barani Afrika katika hali duni na kusababisha ukosefu wa chakula. Umaskini na ukosefu wa usalama wa chakula huwafanya wakulima wadogo kuhamia mijini kutafuta kazi. Katika miji, hata hivyo, mishahara midogo na ajira isiyo rasmi huchangia kwa ukosefu wa usalama wa chakula kwa watu wengi na familia zao, kwa sababu hawawezi kumudu gharama ya chakula bora na cha kutosha (Joubert).

## JE WAJUA? (KIDUNIA)

Tangu miaka ya 1960, jumla ya **chakula kinachozalishwa kote ulimwenguni kimeongezeka, wakati utapiamlo** (undernutrition) umepungua kwa nusu. Lakini sasa, **mara mbili ya watu wana shida ya fetma/vitambi (obesity) kuliko hapo awali.**



Mmoja kati ya kila watu watatu ulimwenguni wanadhaniwa kuwa na lishe duni, kuugua njaa au fetma (Gordon, 2017). Hiyo ni karibu watu milioni 800 ambao wanakabiliwa na njaa ulimwenguni kote, na zaidi ya watu bilioni mbili ambao wana fetma.



Marekani imetumia dola bilioni **50 katika kipindi cha muongo mmoja uliopita kwa ruzuku ya mahindi**, Kiungo cha bei rahisi kinachotumiwa katika soda, lishe ya wanyama na vyakula vingine vya kusindika - kinasaidia kutupa maelezo ya kwanini gharama ya soda imeshuka kwa 33% katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, wakati bei ya matunda nayo imepanda na 40% kwa kipindi hicho



Ifikiapo 2030, inakadiriwa kwamba nusu ya Waafrika watakuwa wanaishi katika miji (kutoka 25% miaka thelathini iliyopita). Mtindo huu wa uhamiaji-mijini unaleta mabadiliko makubwa kwa lishe ya watu na inachangia kupaa kwa viwango vya ugonjwa wa fetma/kitambi/mafuta, ugonjwa wa kisukari na magonjwa mengine yanayohusiana na lishe.



**UZALISHAJI WA CHAKULA NA USAFIRISHAJI HUTUMIA KARIBU THELUTHI YA NISHATI YOTE INAYOTENGENEZA ULIMWENGUNI**


(Barilla)

**TANI BILIONI 1.3, AU KARIBU 30% YA CHAKULA KINACHOZALISHWA KOTE ULIMWENGUNI HUTUPWA KAMA TAKA - KIWANGO AMBACHO KINGELITOSHA KULISHA AFRIKA, ULAYA NA AMERIKA KWA MWAKA MZIMA**



## JE WAJUA? (KIDUNIA)

**BAHARI ZINAANGAMIZWA NA UVUVI WA VIWANDANI**, HASWA BIASHARA KUBWA YA UVUVI MZITO. UVUVI HUO WA KIBIASHARA UNA ALAMA KUBWA YA KABONI, NA INACHANGIA KUPOROMOKA KWA SEKTA YA NDANI YA UVUVI NA KULETA ATHARI MBAYA KWA AJIRA, CHAKULA NA USALAMA WA LISHE.



(DW)

Ulimwenguni kote, tasnia ya chakula inatumia mabilioni ya dola kulenga watoto katika kampeni zao za matangazo na uuzaji. Shirika la Afya Ulimwenguni, WHO, limepaza sauti na kusema inahofia kwamba hii inachangia kuongezeka kwa ugonjwa wa fetma katika watoto, ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu, uharibifu wa maini na magonjwa mengine.



**NCHI ZA KIAFRIKA HUINGIZA CHAKULA CHA TAKRIBAN DOLA BILIONI 35 KILA MWAKA KUTOKA NGA'MBO, LICHA YA UKWELI KWAMBA BARA HILI LINA ARDHI TAJIRI YENYE RUTUBA NA RASILIMALI YA WAFANYAKAZI INAYOPATIKANA KWA UZALISHAJI WA CHAKULA;**

yaani, wakulima ndio wingi wa nguvu-kazi karibu nchini zote. Kuingiza chakula kutoka ng'ambo huchangia mabadiliko ya tabia nchi, na pia humaanisha kwamba fursa muhimu za kutoa ajira kwa vijana katika usindikaji wa chakula hazitengenezwi, wakati akiba za hela za kigeni ambazo zingeweza kutumika kivingine ili kuleta maendeleo pengine zinatumiwa kwa chakula.

## JE, WAJUA? (KWA NCHINI TANZANIA)

KAYA MASIKINI NCHINI TANZANIA hutumia **75% ya mapato yao kwenye chakula.**



(USDA 2015)

**INAKADIRIWA WATANZANIA MILIONI 5 KATI YA MILIONI 48 WALIKABILIWA NA UKOSEFU WA CHAKULA MNAMO MWAKA 2015. WATANZANIA WAPATAO MILIONI 14 WANAWEZA KUKOSA USALAMA WA CHAKULA IFIKAPO MWAKA 2024.**




(USDA 2015)

Kwa wastani mtu wa kawaida wa kijijini, ni aina ya vyakula 15 tofauti hutoa 80% ya kalori za kila siku: mahindi, mchele, maharagwe, matoke, mawele, mtama, viazi, viazi-vitamu, ngano, mihogo, kuku, nyama ya mbuzi, samaki, mafuta ya kupikia, maembe, ndizi zilizoiva na matunda mengine. Kwa Mtanzania wa mijini, vyakula hivi hutoa 67% tu ya kalori za kila siku.

(USDA 2015)

**WATANZANIA HUTUMIA KARIBU MOJA YA TANO YA MAPATO** yao kwenye 'bidhaa zilizofungishwa (consumer packaged goods) kama vile soda au juisi, vinywaji vya nishati na chakula kilichopikwa.



(Nielsen)


Kahawa, korosho, karafuu, tumbaku, mabwawa na magugu-maji (seaweed) ni mfano wa mazao muhimu ya kibiashara ambayo yanatolewa na wakulima wakubwa wa biashara na pia wakulima wa kiwango kidogo. Lakini, hizi bidhaa nyingi husafirishwa nje zikiwa mbichi au bila tija kwa sababu ya ukosefu wa usindikaji wa ndani na maarifa ya kuziongezea thamani. Hii inamaanisha kwamba Tanzania inapoteza thamani ile kubwa ya bidhaa hizo, na kupunguza ukuaji wa uchumi wa ndani na kitaifa, na jamii kuendelea kuwa katika hali ya umasikini.

(African Business)



## JE, WAJUA? (KWA NCHINI TANZANIA)

**MATUMIZI YA PROTINI YA  
WANYAMA NA MAZIWA  
IKO CHINI KOTE TANZANIA.**



(USDA 2015)

Maduka makubwa  
(Supermarkets)  
yanaenea kila mahali  
nchini Tanzania, na  
karibu 45% ya idadi ya  
watu inayafikia/inapata  
huduma katika maduka  
haya.



(Nielsen)

## KUANGALIA KWA UKARIBU UHUSIANO KATI YA USALAMA WA CHAKULA, USTAHIMILIVU WA MABADILIKO YA TABIA NCHI NA SEKTA YA CHAKULA YENYE AFYA

Kuna nguzo nne za usalama wa chakula:

- **Upatikanaji** wa chakula unategemea uzalishaji, usambazaji na ubadilishanaji wa chakula. Hii inamaanisha kuwa na ardhi na maji ya kutosha, na mazingira mazuri ya kukuzia chakula. Inamaanisha pia kuwa na usafirishaji, miundombinu na masoko ipo ili chakula hicho kiweze kuwafikia watu wanaokihitaji.
- **Upatikanaji** wa chakula unategemea kupata chakula kwa njia ya kukikuza/kuzalisha, au kuwezesha kiuchumi kwa kuwa na fedha za kutosha kununua chakula - au mchanganyiko wa yote mawili.
- **Matumizi** ya chakula inamaanisha kwamba chakula kiko salama, na chenye afya na lishe bora. Kwa mfano, kimechakatwa, kutayarishwa na kusindikwa ilivyo muhimu ili kuzuia uchafuzi au uharibifu. Pia inategemea kuwa kile chakula kinafaa tamaduni za watu ili kukidhi matakwa yao. Na inategemea watu kuwa na afya na usafi tosha ili miili yao iweze kuupokea ubora ulio katika kile chakula vizuri, ili kwa mfano, kuzuia kuenea kwa magonjwa na wadudu/vimelea vya tumbo kupitia chakula.

- **Uthabiti/uendelevu** wa upatikanaji, ufikiaji na matumizi ya chakula ni nguzo ya nne ya usalama wa chakula. Watu, kaya na jamii zinahitaji kupata endelevu wa zile nguzo tatu za kwanza, bila usumbufu wowote, ili kuzihirisha kuwa wanao usalama kichakula (Food and Agriculture Organisation of the United Nations).

Sekta ya chakula haiwezi kutengwa na kilimo. Kuwa na sekta bora ya kilimo inaweza kujenga usalama wa chakula na uvumilivu wa mabadiliko ya tabia nchi kwa njia kadhaa. Kuna fursa kubwa zilizopo katika sekta ya kilimo za kutengeneza ajira ambazo zinashirikisha vijana katika ujenzi wa uchumi wa kijani kibichi (greener economy), katika kilimo na kukuza biashara ndogo-ndogo za usindikaji kilimo katika mnyororo wa thamani. Usalama wa chakula haategemei tu uwezo wa wakulima na wafanyabiashara kuzalisha chakula kwa kaya, ila pia kuweza kukabiliana kikamilifu na mabadiliko muhimu kwa sekta ya kilimo ambayo yametokea katika miaka 20 iliyopita, kama vile kuongezeka kwa uchumi wenye misingi ya fedha, kuongezeka kwa utandawazi katika mnyororo wa chakula na bei za chakula zisizotabirika katika masoko ya ndani na ya kimataifa (Committee on World Food Security).

### RASILIMALI



- <http://www.tomatoesandtaxiranks.org.za/chapters/2-big-is-beautiful/>
- Raj Patel 'Cheap Nature, Cheap Food, etc.' <http://rajpatel.org/>
- Food waste <https://www.youtube.com/watch?v=IKNwEUYtDto>
- Impacts of factory farming of animals: <https://www.youtube.com/watch?v=ILhEmGx8YQE>
- Johan Rockstrom: How food connects all the SDGs <https://www.stockholmresilience.org/research/research-videos/2018-08-22-how-food-connects-all-the-sdgs.html>

## NJIA ZA KUZUNGUMZA KUHUSU MFUMO WA CHAKULA

- Ni mabadiliko gani unayoona katika tabia za watu za kula kwenye jamii yako? Kuna ongezeko la maduka ya chakula cha haraka (fast food)? Watu wana mtazamo upi kuhusu ya chakula cha haraka?
- Watu wanapataje chakula katika jamii yako? Kupitia maduka makubwa? Masoko/duka ya mitaani? Moja kwa moja kutoka kwa wakulima? Ni sababu gani zinazochangia aina ya chakula kinachopatikana katika jamii yako, na maamuzi ya watu kuhusu watakavyopata chakula?
- Vyakula vipi vya asili na mazao vinavyopatikana katika eneo lako? Unahisi vipi kuhusu vyakula hivi? Watu katika jamii yako wanavionaje? Unafikiri watu huthamini vyakula hivi, au wangetamani aina nyingine ya lishe? Kwa nini?
- Unaona njia ambazo chakula kinapotezwa/kinatupwa/kinachezewa kwenye jamii yako? Kwa nini hii hutokea, na unaona njia zipi ambazo zinaweza kuizuia?
- Jamii yako unafikiria iko na kiasi gani cha usalama wa chakula? Na kwenye kaya/nyumba yako, je? Nini hufanya watu na kaya wawe na usalama wa chakula au ukosefu huo katika jamii yako? Kuna njia zozote za kuboresha hali ya usalama wa chakula katika jamii yako?
- Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha lishe bora? Watu wanajua kuhusu chakula chenye afya bora? Wanaweza kuvipata vyakula vyenye afya? Kwanini wanaweza na kwanini hawawezi? Na ikiwa hawawezi, basi ni nini watu katika jamii yako wangehitaji ili waweze kupata lishe yenye afya?
- Wengi wa watu hula lishe za aina fulani kwa hiari yao au wanalazimaka? Je, unafikiria watu wanafurahia chakula wanachokula? Kwanini (ikiwa ni ndio/hapana)?
- Watu hula chakula cha haraka katika jamii yako? Kwanini? Ni chakula maalumu sana? Ni aina ya chakula cha kujivunia kwa marafiki zako? Kula katika mgahawa wa chakula cha haraka hukufanya uhisi vipi, kimwili na kihisia?

### TAARIFA PICHA (INFOGRAPHICS)

- **WWF SA Food industry report 2019**  
[https://dtnac4dfluyw8.cloudfront.net/downloads/agri\\_food\\_system.pdf?27341/agri-food-systems-facts-and-futures](https://dtnac4dfluyw8.cloudfront.net/downloads/agri_food_system.pdf?27341/agri-food-systems-facts-and-futures)  
P. 6-7, 13, 17
- <https://www.healthshare.co.za/a-look-inside-the-fast-food-industryuth-africa-infographic/>
- <https://www.dailyinfographic.com/10-companies-that-control-the-food-industry>
- <https://www.columnfivemedia.com/work-items/infographic-9-shocking-facts-about-the-food-industry>
- **Food waste:** <https://za.pinterest.com/pin/165577723773877725/>
- <https://za.pinterest.com/pin/438256607460046855/>



### MAANDALIZI YA KIPINDI

#### MADA MAHUSUSI

#### NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU TASNIA YA CHAKULA

- Ni mabadiliko gani unayoona katika tabia za watu za kula katika jamii yako?
- Kuna ongezeko la maduka ya chakula cha haraka? Watu wana mtazamo upi kuhusu chakula cha haraka?
- Watu wanapataje chakula katika jamii yako? Kupitia maduka makubwa? Soko/maduka ya mtaani? Moja kwa moja kutoka kwa wakulima?
- Ni sababu gani zinazochangia kwa aina ya chakula kinachopatikana katika jamii yako?
- Ni sababu gani zinazochangia maamuzi ya watu kuhusu chakula?
- Ni vyakula gani vya asili na mazao yanayopatikana katika eneo lako? Unahisi vipi kuhusu vyakula hivi? Watu katika jamii yako wanavionaje? Unafikiri watu huthamini vyakula hivi, au wangetamani aina nyingine ya lishe? Kwa nini?
- Unaona njia ambazo chakula kinapotezwa/kutupwa/kuchezewa kwenye jamii yako? Kwa nini hii hutokea, na unaona njia zipi ambazo zinaweza kuizuia?
- Jamii yako unafikiria ina kiasi gani cha usalama wa chakula? Na kwenye kaya yako, je? Nini hufanya watu na kaya wawe na usalama wa chakula au ukosefu huo katika jamii yako? Kuna njia zozote za kuboresha hali ya usalama wa chakula katika jamii yako?
- Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora? Watu wanajua kuhusu chakula chenye afya bora? Wanaweza kufikia/kupata vyakula vyenye afya? Kwanini wanaweza na kwanini hawawezi? Na ikiwa hawawezi, nini watu katika jamii yako wangehitaji ili waweze kupata lishe yenye afya?
- Wengi wa watu hula lishe za aina fulani kwa hiari yao au wanalazimaka? Je, unafikiria watu wanafurahia chakula wanachokula? Kwanini (ikiwa ni ndio/hapana)?
- Watu hula chakula cha haraka katika jamii yako? Kwanini? Ni chakula maalumu? Ni chakula cha kujivunia kwa marafiki zako? Kula katika mgahawa wa chakula haraka (Fast food) hukufanya uhisipi, kimwili na kihisia?

#### CHAGUA MADA MAHUSUSI

Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora?

#### Njia za kuzungumza kuhusu: Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora?

- Ni nini kinachodhaniwa kuwa “lishe yenye afya” katika jamii yako?
- Chakula chenye afya bora kinapatikana katika jamii yako?
- Ni changamoto gani zilizopo katika kutunza lishe yenye afya bora katika jamii yako?
- Ni hatua gani, za kibinafsi au kijamii, zinazoweza kuchukuliwa ili kuboresha ufahamu, maarifa na uelewa wa watu ili wazoe kula vyakula vyenye afya?

**MIUNDO YA VIPENGELE VYA KIPINDI CHA REDIO****SAUTI ZA UMMA****Lengo la sauti za umma**

Kupata maoni mengi kuhusu mada moja

**Utazungumza na nani**

Mtu yeyote kutoka kwa jamii.

**Swali**

Unapendelea kununua chakula cha haraka au kupanda/kulima na kupika chakula chako mwenyewe?

**MAONI YA SAUTI****Lengo la maoni ya sauti**

Kupata maoni ya watu kuhusu mada ambayo wanajali.

**Utazungumza na nani?**

Uliza mtu katika jamii anayelima, kula /kuuza mboga zake mwenyewe atoe maoni yake.

Uliza kijana atoe uzoefu wake wa kula chakula cha haraka dhidi ya kula chakula kilichopikwa nyumbani.

Uliza mfanyakazi wa mgahawa anavyofikiria kuhusu utupaji (uharibifu) wa chakula na athari inayotelea sayari (dunia).

**WASIFU WA SAUTI****Lengo la wasifu wa sauti**

Wasikilizaji wasikie hadithi ya kuhamasisha kuhusu mada ya kipindi.

**Utazungumza na nani?**

Mfanyabiashara binafsi/biashara rejareja ambaye anaweza kutoa uzoefu wake katika kununua na kuuza viwango vikubwa na aina nyingi za chakula. Uliza jinsi wanavyoshughulikia upotezaji/utupwaji/uharibifu wa bidhaa (wastage) na bidhaa zilizoisha muda wake matumizi (expired products).

Mjasiriamali wa ndani ambaye anayelima/panda au kuuza chakula kilichotengenezwa ndani ya jamii yake.

**Maswali**

- Unaona njia zozote ambazo chakula kinapotezwa/kuchezewa/kutupwa katika jamii yako? Kwanini inatokea hivyo, na unaona inaweza kuzuiwaje?
- Watu wanapataje chakula katika jamii yako? Kupitia maduka makubwa? Masoko/maduka ya mtaani? Moja kwa moja kutoka kwa wakulima?
- Ni sababu zipi zinazochangia aina ya chakula kinachopatikana katika jamii yako?
- Je, mambo haya yanaathiri maamuzi ya watu inapofikia swala la watakavyopata chakula?

**Tafadhali angalia maswali ya mahojiano katika sehemu ya “Jinsi ya kuandaa kipindi chako”**



## TANGAZO LA UMMA (PSA)



### Lengo la Tangazo la Umma

Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani. Unda tangazo la umma ambalo linahimiza watu kusaidia ukuzaji/ulimaji wa chakula wa ndani AU kupanua uelewa wao kuhusu kiasi cha nishati na rasilimali ambazo hutumiwa kutunza tasnia ya chakula cha haraka.



**Sauti 1:** Vipi Marie, tafadhali karibu kwangu kwa ajili ya chakula cha mchana mwishoni mwa wiki hii! Tutapika wali na mboga za majani za asili tulizopanda kwenye bustani yetu!

**Sauti 2:** Mmmmm, asante Sara, lakini nitaenda kwenye mgahawa mpya wa chakula cha haraka wa McDonalds kupata chakula changu cha mchana. Wamezindua 'burger' yenye ladha mpya na vijana wote watakuwa huko. Njoo twende pia?

**Sauti 1:** Lo, kwa kweli ningependa kuonja mboga kutoka kwenye bustani yako. Lakini pia, sitaki kukosa kula bata na wenzetu.

**Sauti 2:** Ndio, njoo tu, itakuwa raha sana! Tunaweza kuvaa vizuri.

**Sauti 1:** Sawa, tutaenda pamoja basi!

### Wito/Ujumbe (slogan)

Tabia zetu za kula zinaathiri mabadiliko ya tabia nchi. Ulimwenguni kote, tasnia ya chakula hutumia mabilioni ya dola kwenye kampeni za matangazo na uuzaji zinazolenga watoto. Usiwe mlaji asiyejali. Fikiria kabla ya kununua!

## MAANDALIZI YA KIPINDI CHAKO



**Tumia miundo ya vipengele vya kipindi cha redio, utafiti wako na maandalizi yaliopendekezwa ili kutengeneza kipindi chako.**

[MWANZO:]

**Mtangazaji 1:** Imetimia [TAJA SAA] na karibu ujiunge nasi kwenye makala ya [TAJA JINA LA KIPINDI] hapa [TAJA JINA LA STESHENI]. Mimi ni [TAJA JINA LAKO].

**Mtangazaji 2:** Hiyo ni kweli! Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO]. Kipindi cha leo, tutazungumzia jambo ambalo sote hatuwezi kuishi bila ... chakula! Ndio, wenzangu, mmesikia. Tutazungumza kuhusu jinsi vijana wanavyoweza kupunguza alama zao za kiikolojia kwa kufahamu chakula wanachokula au wasichokula. Tutaangalia upotezaji wa chakula, ukuzaji wa chakula na chakula cha haraka!

**Mtangazaji 1:** Naam! Na pia tutazungumzia umuhimu wa vijana, na watu wote, kuzingatia jinsi wanavyofikiria kuhusu chakula, kutoka kikiwa mbegu hadi kufikia mezani. Taarifa moja ya kuhuzunisha ni kwamba: kaya maskini nchini Tanzania zinatumia karibu 75% ya kipato chao kwenye chakula.

**Mtangazaji 2:** Lo! Chakula kina muhimu mkubwa! Leo, tutalenga watu wanaonunua, kuuza na kuzalisha/kulima chakula katika jamii yetu. Sote tuna kula chakula, lakini ni wangapi wetu tuoju safari ambayo bidhaa hizi zimepitia ili kutufikia, kutoka ukuaji hadi ufungaji na usafirishaji? Na ni wangapi wetu tunafikiria kama ile safari ya chakula kutoka kwa mbegu hadi sahani kwa kweli ni salama kwa dunia yetu? Leo tunasikia sauti za jamii yetu kutuambia jinsi vyombo vya habari vya kijamii, matangazo na chapa vinatumia na watu wote, vijana kwa wazee, katika maisha yetu ya kila siku. Tunakuletea habari muhimu inayohitajika kuanza mazungumzo wazi kuhusu mazuri na mabaya yanayotokana na tasnia ya chakula cha ndani/

nchini/asili.

**Mtangazaji 1:** Hebu tusikie watu wanavyofikiria kuhusu tasnia ya chakula.

[TAJA ANAYEHOJIWA]  
[CHEZ MAHOJIANO]

[KUFUNGA KIPINDI:]


**Mtangazaji 1:** leo, tumejifunza mengi kuhusu tasnia ya chakula nchini Tanzania na njia endelevu zenye watu wote wanaweza kutazama na kuingiliana zaidi na chakula wanachotumia!

**Mtangazaji 2:** Kuelewa alama yako kwa dunia ni muhimu sana kwetu sisi vijana, ili kutusaidia kufanya maamuzi na mipango mizuri ya maisha yetu!

**Mtangazaji 1:** Juma lijalo siku ya [TAJA SIKU] saa [TAJA SAA ZA KIPINDI] tutazungumzia kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri!

## MAANDALIZI YA KIPINDI

Kipindi kamili kuhusu mada ya 'Tasnia Ya Chakula' saa 1




### MAADILI NA IDHINI/ RUHUSA

Maadili na idhini: Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao kibinafsi.



## MAANDALIZI YA KIPINDI

### Kipengele Kijani - dakika 10




### MAADILI NA IDHINI/ RUHUSA

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao za kibinafsi.

# TASNIA YA CHAKULA

## MUONGOZO WA SHUGHULI ZA KIJAMII



### MADA MAHUSUSI

### NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZA KUHUSU TASNIA YA CHAKULA

- Ni mabadiliko gani unayoona katika tabia za watu za kula katika jamii yako?
- Kuna ongezeko la maduka ya chakula cha haraka? Watu wana mtazamo upi kuhusu chakula cha haraka?
- Watu wanapataje chakula katika jamii yako? Kupitia maduka makubwa? Soko/maduka ya mtaani? Moja kwa moja kutoka kwa wakulima?
- Ni sababu gani zinazochangia kwa aina ya chakula kinachopatikana katika jamii yako?
- Ni sababu gani zinazochangia maamuzi ya watu kuhusu chakula?
- Ni vyakula gani vya asili na mazao yanayopatikana katika eneo lako? Unahisi vipi kuhusu vyakula hivi? Watu katika jamii yako wanavionaje? Unafikiri watu huthamini vyakula hivi, au wangetamani aina nyingine ya lishe? Kwa nini?
- Unaona njia ambazo chakula kinapotezwa/kutupwa/kuchezewa kwenye jamii yako? Kwa nini hii hutokea, na unaona njia zipi ambazo zinaweza kuizuia?
- Jamii yako unafikiria ina kiasi gani cha usalama wa chakula? Na kwenye kaya yako, je? Nini hufanya watu na kaya wawe na usalama wa chakula au ukosefu huo katika jamii yako? Kuna njia zozote za kuboresha hali ya usalama wa chakula katika jamii yako?
- Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora? Watu wanajua kuhusu chakula chenye afya bora? Wanaweza kufikia/kupata vyakula vyenye afya? Kwanini wanaweza na kwanini hawawezi? Na ikiwa hawawezi, nini watu katika jamii yako wangehitaji ili waweze kupata lishe yenye afya?
- Wengi wa watu hula lishe za aina fulani kwa hiari yao au wanalazimaka? Je, unafikiria watu wanafurahia chakula wanachokula? Kwanini (ikiwa ni ndio/hapana)?
- Watu hula chakula cha haraka katika jamii yako? Kwanini? Ni chakula maalumu? Ni chakula cha kujivunia kwa marafiki zako? Kula katika mgahawa wa chakula haraka (Fast food) hukufanya uhisi vipi, kimwili na kihisia?

### CHAGUA MADA MAHUSUSI

Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora?

### Njia za kuzungumza kuhusu: Chakula ambacho watu hula kwenye jamii yako kina kiwango gani cha afya na lishe bora?

- Ni nini kinachodhaniwa kuwa “lishe yenye afya” katika jamii yako?
- Chakula chenye afya bora kinapatikana katika jamii yako?
- Ni changamoto gani zilizo katika kutunza lishe yenye afya bora katika jamii yako?
- Ni hatua gani, za kibinafsi au kijamii, zinazoweza kuchukuliwa ili kuboresha ufahamu, maarifa na uelewa wa watu ili wazoe kula vyakula vyenye afya?

## MIUNDO YA SHUGHULI ZA KIJAMII

Tunaweza kutumia vipengele kutengeneza “Kipengele cha tasnia ya chakula/kipengele cha kijani”. Tunapendekeza kipengele kitumie/kishirikishe sauti za watu wengine mitaani na kushirikisha sana waskilizaji katika kipindi.



### **MGENI MZUNGUMZAJI (ALIYE NA UJUMBE MAALUM)**



#### **Lengo la kuwa na mgeni mzungumzaji**

Mgeni aliye alikwa ni mtu ambaye anaweza kushiriki kwa kutoa ujuzi wa kitaalam kuhusu taarifa ya athari au kutoa simulizi yake binafsi kuhusiana na taarifa ya athari

#### **Baadhi ya maswali ambayo mgeni anaweza kutafakari kabla ya mazungumzo:**

- Uhusiano kati ya tasnia ya chakula na mabadiliko ya tabia nchi ni upi?
- Vijana wanafuata kutokana na kuelewa mzunguko wa maisha wa bidhaa za chakula wanazonunua na kutumia?
- Ni mabadiliko gani makubwa, katika tabia za vijana wa kitanzania, ambayo wanahitaji kuyafanya kuhusiana na kununua na kutumia chakula?
- Vijana wanawezaje kuanza kupunguza alama zao za uharibifu na mabadiliko ya tabia nchi kwenye dunia katika suala la ununuzi na matumizi ya chakula?



### **MAHOJIANO**



#### **Lengo la mahojiano**

Mahojiano ni mazungumzo kati ya watu wawili, ambapo maswali yanaulizwa na majibu kutolewa.



#### **Maswali yaliyopendekezwa ya mahojiano na mfanyakazi wa kuzalisha, kutengeneza au kuuza chakula kwenye jamii yako:**

- Alama ya kiikolojia (ecological footprint) kwako inamaanishaje?
- Fafanua uzoefu wako wa “chakula cha haraka”.
- Una mawazo na tabia zipi kuhusu chakula unachokuza/tengeneza /uuza?
- Jinsi unavyokuza / kutengeneza / kuuza chakula ina athirije dunia? (Kwa njia nzuri au hasi?)
- Kwenye jamii unayoishi, ni machaguo gani yaliyopo ya ununuzi wa bidhaa za chakula kutoka kwa wazalishaji wa ndani, wasindikizaji na wauzaji?
- Ni changamoto zipi ambazo vijana wanakabiliwa nazo wakati wanafanya maamuzi ya ununuzi wa chakula?
- Ikiwa vijana wanataka kujifunza mengi zaidi kuhusu mzunguko wa maisha wa bidhaa fulani ya chakula, wanapaswa kwenda wapi?



### **WIMBO MFUPI (JINGLE)**



#### **Lengo la wimbo mfupi (jingle)**

Jingle ni wimbo mfupi (au tune) amabao una ujumbe wazi na ni rahisi kuimba na kukumbuka.

## MIUNDO YA SHUGHULI ZA KIJAMII



### MCHEZO WA KUIGIZA



#### Lengo la mchezo wa kuigiza

Lengo la mchezo wa kuigiza: Kutoa hali ambayo inaruhusu wasikilizaji “kuigiza” jambo kuhusu taarifa muhimu.

Chagua idadi ya wahusika wanaohitajika na wape waigize muongozo na fursa ya kutafsiri taarifa muhimu. Hili ni jambo ambalo waigizaji wenyewe watalifanya.

#### Waigizaji

Khalid, Tumaini

#### Maelezo ya Igizo

Khalid amekasirishwa na mwenzake, Tumaini. Tumaini amekuwa akila chakula cha aina ya ‘burger’ kutoka kwa mnyororo maarufu wa chakula cha haraka kama chakula chake cha jioni kila siku kwa miezi 7 iliyopita. Tumaini haoni shida yoyote, kwani hicho chakula ni cha bei nafuu, huja na kinywaji, katika kifurushi kisafi chenye rangi zinazopendeza na pia chakula hicho humshibisha vizuri. Khalid anasisitiza kwamba sio vizuri kwa Tumaini kuiendeleaza desturi hii, kwa afya yake mwenyewe, na afya ya mazingira. Khalid anaanza kumwelezea sababu zote kwanini hii tabia ina madhara ...



### MAJADILIANO YA JOPO



#### Lengo la majadiliano ya jopo

Mjadala wa jopo unaohusisha kundi la watu kujadili mada moja mbele ya watazamaji. Kuna wakati wa maswali kutoka kwa watazamaji baadaye.



#### Watakao shiriki kwenye majadiliano ya jopo

Mmiliki wa mgahawa, kijana, mjasiriamali ambaye hukuza na kuuza malighafi kwa wazalishaji wakubwa wa chakula, mpishi, mwandalizi.



#### Mifano ya maswali ya kufungua mjadala wa jopo

- Alama ya kiikolojia (ecological footprint) kwako inamaanisha nini?
- Fafanua uzoefu wako wa “chakula cha haraka”.
- Una mawazo na tabia zipi kuhusu chakula unachokuza/tengeneza /uuza?
- Jinsi unavyokuza / kutengeneza / kuuza chakula inaathirije dunia? (Kwa njia nzuri au hasi?)
- Kwenye jamii unayoishi, ni machaguo gani yaliyopo ya ununuzi wa bidhaa za chakula kutoka kwa wazalishaji wa ndani, wasindikizaji na wauzaji?
- Ni changamoto zipi ambazo vijana wanakabiliwa nazo wakati wanafanya maamuzi ya ununuzi wa chakula?
- Ikiwa vijana wanataka kujifunza mengi zaidi kuhusu mzunguko wa maisha wa bidhaa fulani ya chakula, wanapaswa kwenda wapi?

**MIUNDO YA SHUGHULI ZA KIJAMII****JARIBIO****Lengo la jaribio**

Kupima ujuzi wa msikilizaji wako kuhusu mada

**Vitu unavyohitaji kwa zoezi hili**

- Maswali yaliyotayarishwa na majibu
- Zawadi ndogo-ndogo

**Mchakato**

Wasilisha maswali na utoe tuzo/zawadi kwa wale wapatao jibu sahihi. Kutoka kwenye karatasi yenye habari zilizothibitishwa kuwa kweli, tumekuundia maswali mawili yafuatayo ili uyatumie kwenye kipindi chako. Baada ya kutumia haya mawili, jisikie huru kuunda maswali zaidi ili kuwapima wasikilizaji wako!

**Jaribio 1:**

Swali: Kaya masikini nchini Tanzania hutumia kama vile asilimia ... ya mapato yao kwenye chakula.

- A. 3%
- B. 78%
- C. 75%

Jibu sahihi ni C

**Jaribio 2:**

Swali: Watanzania milioni 14 wanaweza kuwa na ukosefu wa chakula kwa mwaka ...

- A. 2024
- B. 2025
- C. 2026

Jibu sahihi ni A

## MAANDALIZI YA SHUGHULI YAKO YA KIJAMII



Tumia miundo ya vipengele na utafiti wako wa kuandika muongozo wako. Hapa kuna mfano wa sehemu ya muongozo. Unaweza kuutumia kama mwongozo unapo tayarisha maandalizi ya shughuli ya kijamii.

### [MWANZO:]

**Mtangazaji 1:** Hamjambo na karibuni! Imetimia [TAJA SAA] na ni saa za [TAJA JINA LA SHUGHULI YAKO YA KIJAMII] hapa [TAJA JINA LA SHULE]. Jina langu ni [TAJA JINA LAKO].

**Mtangazaji 2:** Hiyo ni kweli! Na jina langu ni [TAJA JINA LAKO]. Kipindi cha leo, tutazungumzia jambo ambalo sote hatuwezi kuishi bila ... chakula! Ndio, wenzangu, mmeskia. Tutazungumza kuhusu jinsi vijana wanavyoweza kupunguza alama yao ya kiikolojia kwa kufahamu chakula wanachokula au wasichokula. Tutaangalia upotezaji wa chakula, ukuzaji wa chakula na chakula cha haraka!

**Mtangazaji 1:** Naam! Na pia tutazungumzia umuhimu wa vijana, na watu wote, kuzingatia jinsi wanavyofikiria kuhusu chakula, kutoka kikiwa mbegu hadi kufikia kwenye sahani. Taarifa moja ya kuhuzunisha na kwamba: kaya maskini nchini Tanzania zinatumia karibu 75% ya kipato chao kwenye chakula.

**Mtangazaji 2:** Lo! Chakula kina umuhimu mkubwa! Leo, tutazingatia watu wanaonunua, kuuza na kukuza/kuzalisha chakula katika jamii yetu. Sote tuna kula chakula, lakini ni wangapi wetu tuoju safari ambayo bidhaa hizi zimepitia ili kutufikia, kutoka ukuaji hadi ufungaji na usafirishaji? Na ni wangapi wetu tunafikiria kama ile safari ya chakula kutoka kwa mbegu hadi mezani kwa kweli ni salama kwa dunia yetu? Leo tunacheza sauti za jamii yetu kutuambia jinsi vyombo vya habari vya kijamii, matangazo na chapa vinatumia na watu wote, vijana kwa wazee, katika maisha yetu ya kila siku. Tunakuletea habari muhimu inayohitajika kuanza mazungumzo wazi kuhusu mazuri na mabaya yanayotokana na tasnia ya chakula cha ndani/nchini/asili.

**Mtangazaji 1:** Hebu tusikie watu wanavyofikiria kuhusu tasnia ya chakula.

[CHEZA SAUTI ZILIZOREKODIWA]

[CHEZA MAHOJIANO]

[SHIRIKISHA WASHIRIKI WALIOHUDHURIA KWA KUULIZA MASWALI NA KUWAPA FURSA YA KUTOA MAONI YAO WAZI WAZI]

[FUNGA]

**Mtangazaji 1:** Leo, tumejifunza mengi kuhusu tasnia ya chakula nchini Tanzania na njia endelevu ambazo watu wote wanaweza kuingiliana na chakula wanachotumia!


**Mtangazaji 2:** Ndio! Ni muhimu sana kwetu sisi vijana kuelewa alama yetu duniani ili tuweze kufanya maamuzi na mipango mizuri kwa maisha yetu!

**Mtangazaji 1:** Tukutane tena hivi karibuni! Hadi wakati huo, sikiliza kipindi chetu kila wiki kwenye [TAJA JINA LA STESHENI] saa [TAJA MUDA WA KIPINDI] tutakuwa tunazungumza yote kuhusu [TAJA MADA YA KIPINDI CHA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, Kwaheri!

**MAANDALIZI YA SHUGHULI YA KIJAMII**

Mpango wa maandalizi ya shughuli ya kijamii hukusaidia kuzingatia ratiba ya hafla yako. Ni orodha ya shughuli na mpangilio maalum wa mambo yatakavyotokea katika shughuli yako ya kijamii. Gawa muda kwa kila shughuli ili uweze kuzingatia saa katika maandalizi ya shughuli yako ya kijamii.

Hapa kuna mfano wa ratiba ya shughuli ya kijamii ya saa moja.

**MAADILI NA IDHINI**

Maadili na idhini: Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa wengine, kwa hivyo hakikisha umewafahamisha wasikilizaji wako kuwaheshimu wale watakaotoa simulizi zao binafsi.

Ikiwa kuna taarifa yoyote isiyo sahihi itakayotokea katika muundo wowote kama vile jaribio, kuigiza au majadiliano ya jopo, kanusha taarifa hiyo. Usiruhusu wasikilizaji wako kuondoka na hadithi/taarifa potofu.

Baada ya kukamilisha muongozo wako, kupanga wasanii wako, kuandaa shughuli ya kijamii na miundo yote, ni wakati wa kuanza!